Ni Lazima Mtu awe Mshirika wa Kanisa Ndio Aokolewe?

(Must One be a Member of the Church to be Saved?)

Na

Ellis P. Forsman

Ni Lazima Mtu awe Mshirika wa Kanisa ndio Aokolewe?

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 7, 2011

Ni Lazima Mtu awe Mshirika wa Kanisa Ndio Aokolewe?

Efe. 1:19-23

Efe. 1:19-23, "*Na ubora wa ukuu wa uweza wake ndani yetu tuaminio jinsi ulivyo; kwa kadiri ya utendaji wa nguvu za uweza wake; aliotenda katika Kristo alipomfufua katika wafu akamweka mkono wake wa kuume katika ulimwengu war oho; juu sana kuliko ufalme wote, na mamlaka, na nguvu, na usultani, na kila jina litajwalo, wala si ulimwenguni humu tu, bali katika ule ujao pia; akavitia vitu vyote chini ya miguu yake akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa ambalo ndilo mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote.*"

Misemo iliozoeleka ikisemwa leo ni:

- "Sio lazima mtu awe mshirika wa kanisa ndio aokolewe."
- "Kanisa halimuokowi mtu."
- "Mtu anaweza kuwa Mkristo lakini asiwe mshirika wa kanisa lolote."

Wengine wana mawazo kwamba kuwa raia mwema ni sawa na kuwa Mkristo. Tunapaswa kuangalia kama imani hizi ni za kweli. Je Biblia inafundisha mafundisho haya yaliyozoeleka?

Bwana anaokoa wapi?

Ni ukweli unaokubaliwa na wengi kwamba Biblia inafundisha kwamba Bwana anaokoa.

Je msemo unaweza kupatikana kwenye Biblia, "Watu wema wanaweza kuokolewa nje ya kanisa"?

Swali ni: "Bwana anaokoa wapi – kanisani, au nje ya kanisa? Au "Mtu anaweza kuokolewa nje ya kanisa la Bwana?"

Biblia inajibu swali, sio tu kwamba inafundisha Mwokozi ni nani, lakini pia lini na wapi anapookoa. Mwokozi ndiye aanaye eleza masharti ya kumssikiliza mwanadamu na anamwambia ni kwa njia gani na katika sehemu gani anapaswa kupokea wokovu.

Yesu Kristo ana haki ya kusema yote lini na wapi atakapo okoa.

Bwana anataka wokovu kwa wote; lakini kama mwanadamu anafaa kuipata, basi anapaswa kuingia kwenye ulingo ambao Mungu ameweka.

- 1 Thes. 5:9, "*Kwa kuwa Mungu hakutuweka kwa hasira, bali tupate wokovu, kwa Bwana wetu Yesu Kristo;*"
- 2 Pet. 3:9, "*Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake, kama wengine wanavyodhani kukawia, bali huvumilia kwenu maana hapendi mtu yeyote apotee, bali wote wafikilie toba.*"
- 1 Tim. 2:4, "*Ambaye hutaka watu wote waokolewe, na kupata kujua yaliyo kweli.*"

Mungu "huweka katika uzio" baraka zake

Kwa sababu kadhaa, Mungu mara zote anaona ni vyema kuweka vizuizi au mahitaji ambayo inaondoa yote katika wokovu ambao hautaendana nayo.

Kuelezea: Katika siku za Nuhu, Mungu aliwapa wanadamu wokovu kutoka katika maangamizi ya gharika, lakini zawadi hiyo ilikuwa kwa wale tu waliopenda kuingi kwenye safina kabla ya gharika kuja. Kuhusiana na wokovu huo, Petro aliandika katika 1 Pet. 3:19-20, "*Ambayo kwa hiyo aliwaendea roho waliokaa kifungoni, akawahubiri; watu wasiotii hapo zamaani, uvumilivu wa Mungu ulipokuwa ukingoja, siku za Nuhu, safina ilipokuwa ikitengenezwa; ambamo ndani yake wachache, yaani, watu wanne, waliokokaa kwa maji.*"

Kufungu hiki kinaeleza wazi kwamba wokovu huu ulikuwa kwenye safina. Wote waliokuwa nje ya safina walipotea. Hakukuwa na sehemu nyingine ya kuweza kuokolewa kutoka kwa gharika; hivyo basi, isipokuwa watu wasipoingia kwenye safina wamepotea.

Mwisho wa adithi unaonyesha unaonyesha kwamba ni watu wanane tu ndio waliokolewa na gharika. Hawa waliingia kwenye safina – na wako salama.

Hataivyo, wanadamu wote walishindwa kukidhi mahitaji takatifu kwa kushindwa kuingia ndani ya "kuta" unaozunguka wokovu; hivyo, waliangamizwa.

Kwa vile maagizo ya Mungu katika siku za Nuhu uliweka wokovu kutoka kwa gharika katika safina, swali linafuata, "Mungu ameweka wapi wokovu kutoka katika dhambi?"

Mungu ameweka wokovu na ameweka maagizo fulani kwa viumbe vilivyo na uhai, kama wanapenda kuokolewa.

Watu hawawezi kuupata huo wokovu sehemu nyingine yoyote, au kwa njia yoyote, tofauti na mahitaji haya.

Wokovu upo katika Kristo

Biblia inaeleza wazi kwamba woko upo ndani ya Kristo; na kwamba Mungu anaokoa tu kupitia Kristo.

Mtume Paulo anaeleza katika 2 Tim. 2:10, "*Kwa ajili ya hilo nastahimili mambo yote, kwa ajili ya wateule, ili wao nao waupate wokovu ule ulio katika Kristo Yesu, pamoja na utukufu wa milele.*"

Kwa vile Paulo anasema kwamba wokovu unapatikana "*katika Kristo*", swali linaweza kuulizwa, "Watu hawawezi kuupata wokovu sehemu nyingine?"

Mtume Petro anasema katika Mdo. 4:11-12, "*Yeye ndiye jiwe lile lililodharauliwa naa ninyi waashi, nalo limewekwa kuwa jiwe kuu la pembeni. Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo.*"

Petro anadiriki kueleza wazi, "*Kwa maana hakuna wokovu katika mwingine.*"

Alafu Biblia inaeleza kwa msisitizo kwamba wokovu ni "*katika Kristo*" na sio katika mwingi.

Kwa vile, watu waliovuviwa wa Mungu wanaweka wokovu kutoka dhambini katika sehemu sahihi hakika kama Petro alivyoweka wokovu kutoka katika gharika katika wakati unaofaa.

Mmoja alikuwa "*katika safina*"; na nyingine "*katika Kristo*".

Wokovu leo haupatikani sehemu yoyote ile; inaweza kupatikana "*katika Kristo Yesu*".

Kwa vile, wanadamu wanakosea wanapofikiri kuna njia nyingi zinazoweza kumwokoa mtu.

Hakuna njia elfu zinazompeleka mtu mbinguni, au mbili. Kuna njia moja tu, sio tu ka-njia.

Yesu alisema katika Yohana 14:6, "*...Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima, mtu haji kwa Baba ila kwa njia ya mimi.*"

Hatuwezi kuupata wokovu sehemu nyingine yo yote; maana haipatikani popote isipokuwa "*katika Kristo*". Katika yeye kuna mzunguko ambamo wokovu unapatikana.

Ni baraka zipi zilizomo ndani ya Kristo?

Baraka zote za kiroho ziko ndani ya Kristo. Efe. 1:3, "*Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo aliyetubariki kwa baraka za rohoni, katika ulimwengu wa roho ndani yake Kristo.*"

Angalia baadhi ya baraka nyingi zinazopatikana "*ndani ya Kristo*" na inamanisha nini kuwa "*ndani yake*".

Ukombozi upo ndaani ya Kristo

Rum. 3:24, "*Wanahesabiwa haki bure kwa neema yake, kwa njia ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu.*"

Ukombozi ni neno lingine la wokovu au msamaha. Yesu alikufa kumkomboa mwanadamu kutoka dhambini, lakini mtu ni lazima aje katikati ya mipaka hiyo ambapo ukombozi ulipo ili anunuliwe kwa thamani ya damu yake.

- 1 Pet. 1:18-19, "*Nanyi mfahamu kwamba mlikombolewa si kwa vitu viharibikavyo, kwa fedha au dhahabu; mpate kutoka katika mwenendo wenu usiofaa mlioupokea kwa baba zenu; bali kwa damu ya thamani, kama ya mwana-kondoo asiye na ila, asiye na waa, yaani ya Kristo.*"
- Mdo. 20:28, "*Jitunzeni nafsi zenu na lile kundi lote nalo, ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake, mpate kulilisha kanisa lake Mungu, alilolinunua kwa damu yake mwenyewe.*"

Msamaha uko ndani ya Kristo.

Kol. 1:14, "*Ambaye katika yeye tuna ukombozi, yaani msamaha wa dhambi.*"

Kwa vile "*msamaha wa dhambi*" upo "*katika Kristo*", basi mtu anapaswa kuwa pale ili dhambi zake zisamehewe.

Efe. 1:7, "*Katika yeye huyo kwa damu yake, tunao ukombozi wetu masamaha ya dhambi sawasawa na wingi wa neema yake.*"

Mtu ni "*kiumbe kipya*" katika Kristo

2 Kor. 5:17, "*Hata imekuwa mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya ya kale yamepita tazama yamekuwa mapya.*"

"Kiumbe kipya" ni yule aliyezaliwa upya – yule aliyefanyika Mkristo.

Yohana 3:5, "*Yesu akajibu, Amin, Amin, nakuambia mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu.*"

Lakini mtu hawezi kufanyika kiumbe kipya nje ya Kristo. Pia hawezi kuwa kiumbe kipya nje ya ufalme wa Mungu ambayo ilinunuliwa kwa damu ya Kristo.

Maisha yako ndaani ya Kristo

- Yohan 1:4, "*Ndani yake ndimo mlimokuwa uzima, nao ule uzima ulikuwa nuru ya watu.*"
- 1 Yohana 5:11-12, "*Na huu ndio ushuhuda ya kwamba Mungu alitupa uzima wa milele na uzima huu umo katika Mwanawe. Yeye aliye naye Mwana anao huo uzima; asiye naye Mwana wa Mungu hana huo uzima.*"

Hatuwezi kufurahia maisha ya kiroho na wakati uo huo tuwe nje ya mipaka inapo patikana.

Kueleza tena:

- Hapo mwanzo Mungu alitoa uhai kwa viumbe vyote.
- Alichagua kwamba ssamaki waishi majini (Mwan 1) je samaki anaweza kuishi nje ya maji? Hapana, samaki ni lazima waishi katika mipaka hiyo ambapo Mungu aliweka maisha yake.
- Sasa, angalia inavyotumiwa: Ni wapi ambapo Mungu aliweka maisha ya kiroho? Hakika, haikuwa nje ya Kristo, bali "ndani yake".
- Uzima wa milele uko katika Kristo, na kila mtu alieye na Mwana ana uzima pia uliomo ndani ya Mwanaye. Hivyo, mipaka ya maisha ya kiroho ya mwanadamu ni "*katika Kristo*".

Mtu anapatanishwa katika Kristo

2 Kor. 5:18-20, "*Lakini vyote pia vyatokana na Mungu, aliyetupatanisha sisi na nafsi yake kwa Kristo, naye alitupa huduma ya upatanisho; yaani Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake asiwahesabie makosa yao; naye ametia ndani yetu neno la upatanisho. Basi tu wajumbe kwa ajili ya Kristo, kana kwamba Mungu anasihi kwa vinywa vyetu; twawaomba ninyi kwa ajili ya Kristo mpatanishwe na Mungu.*"

Upatanishi ni neno lingine inayoonyesha huruma, msamaha wa dhambi, aau wokovu.

Mwanadamu anapopatanishwa na Mungu, dhambi zake husamehewa, na anaungana na Mungu.

Mungu na mwanadamu hukutana "ndani ya Kristo"; kwa vile, kuwa "ndani ya Kristo" ni kupatanishwa na Mungu.

Mtu hupatanishwa <u>katika</u> mwili

Efe. 2:16, "*Akawapatanisha wote wawili na Mungu katika mwili mmoja, kwa njia ya msalaba, akiisha kuufisha ule uadui kwa huo msalaba.*"

Hivyo basi, mtu ni lazima awe katika mwili huo mmoja ili apatanishwe kwa Mungu; na kuwa katika mwili mmoja ni kuwa "katika Kristo".

Kuwa "katika Kristo" ni kuwa katika kanisa

Biblia inaeleza kwamba "*mwili mmoja*" ni kanisa.

- Efe. 1:22-23, "*Akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akwmweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa ambalo ndilo mwili wake ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote.*"

- Kol. 1:18, "*Naye ndiye kichwa cha mwili, yaani cha kanisa naye ni mwanzi, ni mzali wa kwanza katika wafu, ili kwamba awe mtangulizi katika yote.*"
- Kol. 1:24, "*Sasa nafurahia mateso niliyo nayo kwa ajili yenu; tena nayatimiliza katika mwili wangu yale yaliyopungua ya mateso ya Kristo, kwa ajili ya mwili wake, yaani kanisa.*"

Hivyo, kuwa "*katika Kristo*" ni kuwa katika kanisa lake

Ebu tuyaweke haya pamoja.

Kwa vile kupatanishwa kwa Mungu inamanisha msamaha wa dhambi, watu wanaokolewa, au wanasamehewa, au wanapatanishwa katika kanisa.

Kwa vile watu wanapatanishwa katika mwili mmoja, na mwili ni kanisa, hivyo watu uokolewa, au wanapatanishwa tu katika kanisa, mwili mmoja.

Biblia pia inasema kwamba Kristo ni mwokozi wa mwili, ambayo ni kanisa.

- Efe. 5:23, "*Kwa maana mume ni kichwa cha mkewe, kama Kristo naye ni kichwa cha kanisa; naye ni mwokozi wa mwili.*"
- Efe. 5:29-30, "*Maana hakuna mtu anayeuchukia mwili wake po pote; bali huulisha na kuutunza kama Kristo naye alivyolitendea kanisa. Kwa kuwa tu viungo vya mwili wake.*"

Kwa vile kanisa ni mwili wa Kristo, na Kristo ni Mwokozi wa mwili, inakuaje, mtu anaokolewa na asiwe mshirika wa kanisa? Ni lazima mtu awe mshirika wa kile ambacho Kristo ni Mwokozi ili aokolewe.

Wokovu umeahidiwa kwa wale tu walioko katika mwili wa Kristo, kanisa. Mdo. 2:47, "*Wakimsifu Mungu na kuwapendeza watu wote Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa.*"

Kifungu hiki kinafundisha kwamba Bwana aliwaokoa watu na akawazidisha katika kanisa kwa mfumo uleule.

- Kuokolewa ni kuwa "*katika Kristo*", maana wokovu ni "*katika Kristo*" (2 Tim.2:10.
- Kuokolewa ni sawasawa na kuwa ndani ya kanisa, maana Bwana huwazidisha wale wanaokolewa katika kanisa.
- Hivyo basi, kuwa "*katika Kristo*" ni kuwa katika kanisa lake.

Hakuna watu waliookolewa walipo nje ya kanisa la Agano Jipya kwa sababu Bwana anawazidisha wote waliookolewa katika kanisa.

Kristo alianzisha kanisa moja tu

Biblia inafundisha kwamba kunaa mwili mmoja tu

- 1 Kor. 12:20, "*Lakini sasa viungo ni vingi ila mwili ni mmoja.*"
- Efe. 4:4, "*Mwili mmoja, Roho mmoja, kama na mlivyoitiwa katika tumaini moja la wito wenu.*"
- Mdo. 4:10-12, "*Jueni ninyi nyote na watu wote wa Israeli ya kuwa kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti, ambaye ninyi mlimsulubisha na Mungu akamfufua katika wafu, kwa jina hilo mtu huyu anasimama ali mzima mbele yenu. Yeye ndiye jiwe lile lililodharauliwa na ninyi waashi, nalo limewekwa kuwa jiwe kuu la pembeni. Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo.*"

Biblia pia inafundisha kwamba kuna njia moja tu ya kuingia katika mwili huo.

- Rum. 6:3, "*Basi ndugu chagueni watu saba miongoni mwenu, walioshuhudiwa kuwa wema wenye kujawa na Roho, na hekima ili tuwaweke juu ya jambo.*"
- Gal. 3:27, "*Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo.*"
- 1 Kor. 12:13, "*Kwa maana katika Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kuwa mwili mmoja, kwamba tu Wayahudi au kwamba tu Wayunani; ikiwa watumwa au ikiwa tu huru; nasi sote tulinyweshwa Roho mmoja.*"
- Ufu. 14:13, "*nikasikia sauti kutoka mbinguni ikisema, andika, heri wafu wafao katika Bwana tangu sasa. Naam, asema Roho wapate kupumzika baada ya tabu zao; kwa kuwa matendo yao yafuatana nao.*"

Hitimisho

Mtu anafanyikaje mshirika wa kanisa? Mtu ni lazima afanyike Kristo.

Zifuatazo ni hatua muhimu zinazofanya hilo liwezekane:

- **Imani.** Waeb. 11:6*, "Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa dhawabu wale wamtafutao."* Nilipokuwa shuleni (nikiwa na miaka 17), kijana mmoja jirani yangu mwaka sawa na mimi akniambia kwamba haamini kwamba Mungu yuko. Kwa vile nilisha batizwa, nilichukua nafasi ya kuongea naye kuhusu mandiko. Akaniambia kwamba anaweza kuona kwamba kuishi maisha ya ukristo ni nzuri, lakini hakuwa na uhakika kwamba Mungu yuko. Lakini ili kuwa upande salama, labda anapaswa kwenda kanisani, na akifa na kusimama mbele za Mungu (kama kuna Mungu) siku ya hukumu (kama kuna hukumu), labda kama Mungu akiona kuwa amekwenda kanisani atampeleka mbinguni (kama kuna mbingu), na si motoni (kama kuna moto). Nikamwambia, "haifanyi kazi kwa njia hiyo. Lazima uamini katika yeye kwa moyo wako wote la sivyo huwezi kumpendeza.

- **Toba.** Matend. 2:38*, "Petro akawambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina lake Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi zenu nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."*

  Matend 11:18*, ".....Basi Mungu amewajalia hata mataifa nao <u>toba liletalo uzima."</u>*

  Kama ulikuwa unalala, ukasikia kelele kwenye chumba kingine, na unafikiria mwenyewe, "Kwamba kuna mwizi!" taratibu unachukua simu ya mkononi, unawapigia polisi. Kidogo polisi wanafika na kumshika mwizi. Alafu anapiga kelele, "samahani; samahani!" Anaomba msamaha wa nini? Kwa sababu amekamatwa; si kwamba ameiba. Toba iliyokweli ni kwamba mwizi angeomba msamaha kwamba hataiba tena. Hiyo ndio toba ya kweli. Ni badiliko la nia linaloleta badiliko la matendo. Tunatakiwa kufanya hivyo kabla hatujawa wakristo.

- **Kukiri.** Waru. 10:9-10*, "Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana <u>kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu."</u>*

  Tuna kiri nini? Kwamba tuna amini kwamba Yesu Kristo ni mwana wa Mungu.

Kumbuka kwamba katika andiko hilo hapo juu kwamba imani (kuamini), toba, na kukiri ni "**KATIKA**" haki, uzima, au wokovu. "Katika" inamanisha kuelekeza kwenye kitu Fulani; si kwamba mtu ameshapata.

- **Ubatizo.** Ni katika ubatizo ndipo haki, uzima, na wokovu vinapatikana. Yesu mwenyewe alibatizwa kuitimiza haki yote, *"Lakini Yohana alitaka kumzuia akisema, mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia kubali hivi sasa, kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini, na tazama mbingu zikamfunukia akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema, huyu ni mwanangu mpendwa, ninaye pendezwa naye."* (Math. 3:14-17). Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema ni jambo sahihi la kufanya. Unaona ni jinsi gani ilivyompendeza Mungu Yesu alipobatizwa? Yesu pia akasema, "*Imekuwa kwetu <u>**sisi**</u> kuitimiza haki yote."* Tuna batizwa kwa sababu inatimiza haki yake yote, si kwa sababu ni haki yetu.

  Kwa kweli, tusipo batizwa, tungali katika dhambi zetu. *"Petro akawambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina lake Yesu Kristo <u>kwa ajili ya ondoleo la dhambi</u>, na mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."* (Matend. 2:38). Petro, umesema kusudi la ubatizo ni nini? "*<u>Kwa ajili ya ondoleo la dhambi</u>*". <u>Kwa nini watu wanapenda kuach hatua inayotuondoa dhambi zetu?</u>

Yesu aliamuru kwamba ili kuufikia wokovu lazima tubatizwe. *"Na akawambia enendeni ulimwenguni kote mkahubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye **na** kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa."* (Marko 16:15-16).

Anania alimwambia Sauli (kabla hajaitwa Paulo) kitu iki hiki, "*Unakawilia nini? Simama, na ubatizwe, na uoshwe dhambi zako, ukiliitia jina la Bwana."* (Matend. 22:16). Ubatizo ni hitaji lililotolewa na Mungu.

Ubatizo unaitwa maziko, *"Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima."* (Waru. 6:4). Utu wetu wa kale umekufa. *"Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake. Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlvyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika katika mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili ya kuwa utuwetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusiitumikie dhambi tena."* (Waru. 6:3-6). Ubatizo ni ramani ya Mungu inayotumiwa na damu ya Kristo katika maisha yetu kwa ubatizo. Tunakuwa huru na dhambi zetu za zamani kama tu tukibatizwa.

Hii haimanishi "kunyunyiza. Andiko hilo hapo juu linasema ubatizo ni maziko. Hatuwezi kupeleka maiti makaburini, na kumwekea udongo kidogo juu yake; tunauzika mwili.

Kama hujafanyika Mkristo, kwa nini usifanyike leo?